OFISI YA RAIS-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# HALMASHAURI YA WILAYA KIBAHA

# SHULE YA SEKONDARI RAFSANJANI SOGA

SIMU NA 0713-709354 MKUU WA SHULE,0787-143294MAKAMU WA MKUU WA SHULE

S.L.P. 30288,

KIBAHA.

TAREHA……………………

KUMB. NA. RAFSS/J.1/F.5/2022

MWANAFUNZI ___________________________

S.L.P. ____________

______________________

# YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE</u>

1.0. UTANGULIZI

Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule ya sekondari Rafsanjani Soga mwaka 2022/2023 katika Tahasusi/ combination **HGK/CBG** Unapaswa kufika shuleni tarehe ……………………………… kabla ya saa 11 jioni.

11. JINSI YA KUFIKA SHULENI

Shule ipo Kata ya Soga, Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha Mkoa wa Pwani, Ukitoka Morogoro au Dar es salaam utashuka kituo cha Bus Kongowe (Kibaha) utaona kibao cha shule ya Sekondari Rafsanjani Soga. Usafiri wa kufika shuleni unapatikana, nauli ni kati ya Tshs 1,000 kwa gari na Tshs 3,000/= kwa Pikipiki



Edit with WPS Office

## 2.0. ADA NA MICHANGO YA SHULE

| S/N | MICHANGO | KIASI Tshs |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya shule | 70,000.00 kwa mwaka<br>35,000.00 kwa muhula |
| 2. | Taaluma | 20,000.00 kwa mwaka |
| 3. | Tahadhari | 5,000.00 (haitarejeshwa) |
| 4. | Mpishi na ulinzi | 30,000.00 kwa mwaka |
| 5. | Matibabu (huduma ya kwanza) | 10,000.00 kwa mwaka |
| 6. | Ukarabati wa samani | 15,000.00 Mara moja |
| 7. | Mtihani wa mock | 20,000 Mara moja |
| | JUMLA KUU NI Tshs | 170,000.00 |

NB: *Malipo yote yalipwe katika akaunti ya shule ya NMB* , 21203500177, RAFSANJANI SOGA SECONDARY SCHOOL *kisha mwanafunzi aje na stakabadhi za malipo (Bank pay in slip) ikionyesha jina kamili la mwanafunzi na kidato siku anaporipoti shuleni.*

## 3.0. SARE YA SHULE

3.1. Sketi mbili (2) za rangi ya Bluu bahari (Light bluu – kitambaa kimeambatanishwa). Mshono wa Sketi ni wa rinda Box yenye urefu wa kuvuka magoti.

3.2. Mashati meupe (Tomato) ya mikono mirefu mawili (2).

3.3. Soksi nyeupe ndefu jozi mbili (2).

3.4. Sweta yenye shingo V ya rangi ya blue kwa wanaohitaji.

3.5. Tai itapatikana shuleni

3.6. Viatu vyeusi vya kamba jozi mbili visiwe na urembo

3.7. Truck Suit ya rangi ya bluu bahari na nyekundu zenye ufito mweupe zisizobana kwa ajili ya kuvaa usiku wakati wa kujisomea (Preparation). Na wakati wa mchakamchaka.



Edit with WPS Office

NB: *Kwa waumini wa dini ya Kiislam wanaopenda kuvaa hijabu wanaruhusiwa kwa kuzingatia mshono na rangi zilizotajwa hapo juu.*

## 4.0. MAHITAJI MENGINE

4.1. Bunda (Ream) za karatasi mbili (2) kwa mwaka.

4.2. Raba nyeusi za michezo jozi moja (1).

4.3. Shuka nne (4) za rangi ya pinki.

4.4. Godoro linakodishwa shuleni kwa sh. 10,000.00 kwa mwaka mmoja.

4.5. Mto na foronya.

4.6. Chandarua ya kuzuia mbu rangi nyeupe.

4.7. Ndoo 2 zenye mifuniko kwa ajili ya kutunzia maji.

4.8. Vyombo vya chakula (sahani,yenye vyumba vyumba kikombe, kijiko na chupa ya chai ndogo)

4.9. Tochi ya betri au taa ya Solar kwa tahadhari ya umeme ukikatika.

4.10. Madaftari makubwa (counter book) sita (6).

4.11. Scientific calculator (kwa ajili ya wanafunzi wa sayansi tu).

4.12. Kitambulisho cha bima ya afya kama unacho.

4.13. Nakala ya hati ya cheti cha kuzaliwa.

4.14. Hati ya matokeo ya kidato cha nne.

4.15. Saa ya mkononi

4.16. Dissection kit, Tray na Koti (Lab coat) nyeupe kwa matumizi ya maabara masomo ya Sayasi.

4.17. Fomu ya maelezo ya Daktari kuhusu afya yako ikiwa imejazwa na Daktari (imeambatanishwa).



Edit with WPS Office

4.18. Fomu ya kukubali kujiunga na shule ikiwa imejazwa (imeambatanishwa).

4.19. Sheria za Shule, hakikisha umezisoma na kuzielewa (zimeambatanishwa)

## 5.0. VIFAA VYA USAFI

Vifaa vya usafi (kwanja, panga,jembe, reki, mfagio wa nje) unapaswa kuleta shuleni.

## 6.0. MENGINEYO

6.1. Mwanafunzi awe na t-shirt yenye nembo ya shule(sample inapatikana shuleni)

6.2. Picha na Kitambulisho sh. 6000.00.

6.3. Nembo sh. 2000.00

6.4. Sanduku la bati (Tranka).

6.5. Ni jukumu la mzazi mlezi kugharamia usafiri wa kuja shuleni pamoja na kurudi nyumbani pia kumpatia Mwanafunzi fedha za kutosha za matumizi binafsi awapo shuleni.

6.6. Kipindi chote mwanafunzi awapo shuleni fedha za matumizi binafsi zitumwe kwenye namba hizi TIGO PESA 0710-410132,jina KOKU NGIMBWA. Mzazi/ Mlezi baada ya kutuma pesa taja jina la mzazi, kidato na kiasi ulichotuma.

6.7. Nguo za nyumbani haziruhusiwi. Mwanafunzi aje na sketi nyeusi mbili au zaidi za kushindia zenye marinda box. Vifaa binafsi mfano taulo, kandambili, nguo za ndani, kanga/kitenge n.k.

6.8. Haturuhusu kusuka nywele.

*Nakutakia maandalizi mema*

*Karibu sana Rafsanjani Soga Sekondari*

…………………………

KOKU NGIMBWA



Edit with WPS Office

MKUU WA SHULE

*KIAMBATANISHO A*

RAFSANJANI SOGA SECONDARY SCHOOL P.O.BOX 30288, KIBAHA
STUDENT'S MEDICAL EXANINATION FORM.

TO THE MEDICAL OFFICER IN CHARGE
……………………………………………..
…………………………………………….
…………………………………………….

Please, examine the under named student and note any medical complications towards her joining this school.

Student's name …………………………………… age ………… Class ………

………………………………
HEADMISTRESS

RAFSANJANI SOGA SECONDARY SCHOOL

1. Blood (any infection noted) ………………………………………………………………. Blood group ……………………………………………………………………………………………………………...
2. Stool …………………………………………………………………………………………………….
3. Urine analysis ………………………………………………………………………………………… (note pregnancy) ………………………………………………………………………………………..
4. Eyes (any aye defect) ……………………………………………………………………………………
5. Ears (hearing strength) ……………………………………………………………………………………
6. Chest ……………………………………………………………………………………………………
7. Abdomen ………………………………………………………………………………………………



Edit with WPS Office

8. Hearing diseases ……………………………………………………………………………………………

Any chronic complaints which needs attention of the school authority

……………………………………………………………………………………..……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………..

Name of the medical officer ………………………………………………………..
Designation …………………………………………Signature ……….…………
Station ………………………………………………. Date ………………………

Official stamp ………………………

*KIAMBATANISHO B*

HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBAHA

(ANUANI YA MZAZI)

………………………………………………………………

………………………………………………………………

………………………………………………………………

YAH: <u>HATI YA KUKUBALI MASHARTI KUHUSU MTOTO WANGU</u>

<u>KUSOMA SHULE YA RAFSANJANI SOGA SEKONDARI</u>.

Mimi ……………………………………………………………………………….………………... (Jina la Mzazi/ Mlezi wa mwanafunzi), Mzazi/ Mlezi wa …………………………………………..………………… (jina la mwanafunzi).
Aliye kuwa akisoma shule ya ……………………………………………………… (taja jina la shule aliyosoma mwanafunzi) katika wilaya ya …………………………….……………..
Mkoa wa ………………………………… Ninakubali mtoto wangu asome shule ya sekondari Rafsanjani Soga iliyoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha na nitazingatia sheria, kanuni na taratibu zote za shule



Edit with WPS Office

kama zilivyoelekezwa katika fomu mbalimbali na kwamba:-

1. Mtoto wangu atahudhuria masomo kama kawaida na kufanya shughuli nyingine zote za shule akikaa shuleni/ nyumbani kwa kipindi chote cha miaka miwili cha kidato cha tano hadi cha sita,

2. Kwa muda wote huo wa miaka miwili sita msumbua Mkuu wa shule, Afisa Elimu Sekondari Wilaya na Mkoa kuomba uhamisho.

……………………………… ……………………….

SAHIHI YA MZAZI TAREHE

*KIAMBATANISHO C*

## FOMU YA KIAPO CHA MWANAFUNZI CHA KUTOSHIRIKI MIGOMO, FUJO PAMOJA NA MAKOSA YA JINAI.

Mimi………………………………………………………………………………………………..…..Nimekubali nafasi niliyopewa katika shule ya sekondari Rafsanjani Soga. Ninaahidi kuwa mtiifu na kufuata kikamilifu **SHERIA, KANUNI** na **TARATIBU** halali zilizopo. Pia ninaahidi kufanya bidii na kushirikiana na uongozi wa shule na wanafunzi wenzangu katika kuendeleza taaluma na shughuli nyingine nitakazopangiwa. Naahidi kutoshiriki katika migomo, fujo pamoja na makosa ya jinai.

JINA LA MWANAFUNZI SAHIHI

……………………………………………………………………. ……………………..

Tarehe: …………………………………………….………..

**Nakala:** 1. Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya Kibaha,
S.L.P. 30153,
**KIBAHA.**

2. Afisa Elimu Mkoa,
S.L.P. 30080,



Edit with WPS Office

KIBAHA – PWANI.

3. Mkurugenzi,
Elimu ya Sekondari,
Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa,
DODOMA.

4. Mkurugenzi,
Elimu ya Sekondari,
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Elimu ya Ufundi,
S.L.P. 9121,
DAR ES SALAAM.

*KIAMBATANISHO D*

## FOMU YA TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI

1. Jina kamili la mwanafunzi ……………………………………………………...……………………………
   Dini ………………………………………………………………………………………………………………
2. Tarehe ya kuzaliwa……………………………………Mahali alipozaliwa …………………………………
3. Jina la Baba …………………………………………………………………….……………………Hai/amefariki
4. Jina la Mama………………………………………………………………………………………..…Hai/amefariki
   (a) Je unaishi na wazazi wako? Ndiyo/Hapana
   (b) Kama hapana. Je unaishi na nani?
   Jina ……………………………………………………………………………………….……………………
   Uhusiano ………………………………………………………………………….…………………….
5. Kidato unachokuja kuingia hapa shuleni ……………………………………………………….…………
6. Michezo/ngoma unazopendelea hapa shuleni……………………………………………….……………….
   ……………………………………………………………………………………………………….……….
7. Je umewahi kuwa kiongozi/Kiranja? Ndiyo/Hapana. Kama jibu ni ndiyo eleza ulikuwa kiongozi/Kiranja wa nini? …………………………………………………………………………………………………………
8. Taja mambo mengine unayopendelea kufanya nje ya masomo.………………………………………..
   ……………………………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………………………………

9. ORODHESHA MAJINA YA NDUGU WA KARIBU (WA KIKE/KIUME)

| Na. | Jina la Ndugu | uhusiano | Kazi yake | Na. ya Simu |
|---|---|---|---|---|



Edit with WPS Office

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |

*Nathibitisha kwamba taarifa nilizotoa hapo juu ni sahihi.*

Sahihi ya Mwanafunzi______________________ Tarehe:___________

*KIAMBATANISHO E*

# SHERIA ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sharia ya Elimu Na. 25 ya Mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sharia Na 10 ya mwaka 1995.Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na Mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi wa uendeshaji Elimu .

Unatakiwa kuzingatia sheria ,taratibu,na kanuni za shule kama ifuatavyo;

a) Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanya kazi wote wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
b) Mahudhurio mazuri katika vipindi vyote vya darasani kulingana na ratiba ya shule
c) Kushiriki kwa makini manda
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazo pewa
e) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
f) Kutunza mali ya umma
g) Kumwabudu Mungu kwa utaratibu wa vipindi vya dini vilivyopangwa na shule
h) Ni muhimu na wajibu wa kila mwanafunzi kutii kengele ya shule
i) Ni marufuku kwenda kwenye nyumba za walimu bila kibali maalumu na kuonekana nje ya shule
j) Ni marufuku kwa wanafunzi kuonekana kwenye nyumba za kulala wageni/gesti
k) Ni marufuku kwa mwanafunzi kutumia vipodozi vya aina yeyote na pafyumu.



Edit with WPS Office

l) Ni marufuku kwa mwanafunzi kuonekana ndani au maeneo ya mabweni ya jinsia tofauti
m) Ni marufuku kwa mwanafunzi kushiriki/kushawishiVitendo vyovyote vya mgomo au aina yeyote vya kutowesha Amani shuleni
n) Ni marufuku kuja na vyakula ama vinywaji vya aina yeyote shuleni

# MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE/KUSIMAMISHWA MASOMO.

i. Wizi
ii. Uasherati na ushoga
iii. Ubakaji
iv. Ulevi
v. Kupigana na kupiga
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
vii. Kudharau bendera ya Taifa
viii. Kuoa /kuolewa
ix. Kutoa mimba
x. Kuwa na simu ya mkononi
xi. Kukataa adhabu kwa makusudi
xii. Kugoma ,kuchochea ,kuongoza na kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu



Edit with WPS Office